



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 23 Februari, 2018.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya mwaka 2017/2018.

II. MASWALI:

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

53. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi,
Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kwa kuwa Program ndogo ya utaratibu wa huduma za uhifadhi wa jamii ilipokea maombi 19 mapya kwa wafanyakazi walioumia kazini kwa Unguja na Pemba na kwa sababu dhamira halisi ya program ni kutoa huduma kwa makundi yanayoishi katika mazingira magumu.

- (a) Je kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni makundi mangapi ya watu wanaoishi katika mazingira magumu yaliofaidika na mpango na ni kiasi gani cha fedha kilitumika kusaidia makundi hayo.
- (b) Je maombi 19 mapya yaliyopokelewa mwaka 2016/2017 Wizara imeshalipa kiasi gani cha fedha kwa waathirika hao na ni waathirika wangapi ambao hadi sasa hawajalipwa.
- (c) Kwa kuwa hadi kufikia mwezi Mei, 2017 kulikuwa na deni la zamani la shilingi. 30,607,830/= ambalo lilikuwa ni bakaa ya deni la waathirika wa ajali kazini waliotangulia, je tayari Wizara imeshalilipa na kama bado, ni lini deni hilo litalipwa kwa waathirika hao.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

61. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Chekechea ya Madungu ambayo ina muda zaidi ya miaka 30 tokea ilipojengwa, ina changamoto nyingi ikiwemo ubovu wa majengo yake na idadi kubwa sana ya wanafunzi katika madarasa.

- (a) Je, Serikali inazijua changamoto zilizomo katika skuli hiyo.
- (b) Je, Serikali ina mpango gani kuhusu skuli hiyo katika kuongeza madarasa au kujenga ya ghorofa.
- (c) Je, Serikali isipochukua hatua za haraka za kudhibiti majengo hayo, si utakuwa ule msemo “usipoziba ufa utajenga ukuta”.

Wizara ya Afya:

51. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na ugatuzi kwa ngazi za Wilaya kwa baadhi ya Wizara za Serikali ikiwemo Wizara ya Afya.

- (a) Je ni vituo vingapi vya afya vilivyogatuliwa kwa Unguja na Pemba.
- (b) Je ni changamoto gani zilizojitokeza baada ya kugatuliwa vituo hivyo.
- (c) Je ni upi wajibu wa Wizara ya Afya na ule wa Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa vituo vilivyogatuliwa ili kuviwezesha vituo hivyo kutoa huduma bora kwa wananchi wetu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

68. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kisiwa cha Pemba kimekuwa na changamoto ya usafiri wa anga na wa bahari kwa kukosekana kwa boti zinazoenda kwa kasi na ughali wa usafiri wa ndege.

- (a) Je, Serikali imeliona hilo na kama wanaliona wamechukua hatua gani.
- (b) Kama sekta ya usafiri wa boti za haraka hakuna mwekezaji, je Serikali ina mpango gani wa kununua boti za kasi.
- (c) Je, Serikali inapanga nauli za meli na ndege au wamiliki wanajipangia wenyewe tu.

71. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHANI SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kumekuwa na changamoto ya kuchelewa kutengenezwa kwa meli ya abiria ya Serikali pale inapoharibika na hivyo kuleta usumbufu mkubwa kwa wananchi ambao wanaitegemea sana meli hiyo kutokana na urahisi wa bei na uhakika wa safari.

- (a) Je, ni sababu zipi zinazoifanya meli hiyo kuchelewa kutengenezwa au kupatikana kwa vipuri vyake.
- (b) Je, meli hii iliyonunuliwa haikuletwa na vipuri vya akiba ambavyo ni rahisi kuharibika (Spea).
- (c) Je, kwa vile tumeona changamoto nyingi za kuharibika kwa meli yetu, Serikali imechukua hatua gani za dharura za kuona vifaa gani ni muhimu vya kununua na kuweka katika ghala yetu ya akiba kwa ajili ya meli yetu.

III. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Ripoti ya Kamati ya Bajeti ya mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
23 Februari, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.